

TANGAZO



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



Katibu Mtendaji, Baraza la Mitihani la Tanzania anapenda kuwajulisha watu wote wanaotarajia kufanya Mtihani wa **Kidato cha Nne (CSEE)** na **Maarifa (QT) Novemba, 2022** kama Watahiniwa wa Kujitegemea kwamba;

1. Kipindi cha kawaida cha Usajili kitaanza tarehe **01/01/2022** kwa ada ya Shilingi **50,000/=** kwa wanaojisajili **CSEE** na Shilingi **30,000/=** kwa wanaojisajili **QT** na kitaishia tarehe **28/02/2022**. Aidha, watakojisajili kwa **kuchelewa** kuanzia tarehe **01/03/2022** hadi tarehe **31/03/2022** watalipa Shilingi **65,000/=** kwa Watahiniwa wa Kidato cha Nne (**CSEE**) na Shilingi **40,000/=** kwa Watahiniwa wa Mtihani wa Maarifa (**QT**) ikiwa ni ada ya kawaida pamoja na faini.
2. Mtahiniwa atakayejisajili kufanya Mtihani wa Kidato cha Nne (**CSEE**) **2022** ni yule ambaye anarudia Mtihani wa **Kidato cha Nne (CSEE)** au amefanya na kufaulu Mtihani wa **Maarifa (QT)** katika kipindi kisichozidi miaka **mitano (5)** iliyopita **au** mwenye sifa zinazolingana na hizo alizopata kutoka nje ya Nchi na kufanyiwa ulinganifu na Baraza la Mitihani la Tanzania.
3. Mtahiniwa atakayejisajili kufanya Mtihani wa Maarifa ni yule ambaye anatafuta sifa ya kufanya Mtihani wa Kidato cha Nne kama Mtahiniwa wa Kujitegemea.
4. Usajili unafanyika kwa njia ya mtandao, kwa kufuata hatua zifuatazo;
 - (a) Fika Kituo utakachofanyia Mtihani ili kupata namba rejea (Reference Number) ambayo inatolewa bure.
 - (b) Fika Ofisi ya Posta kupata 'Control Number' ya kufanyia malipo ya ada ya Mtihani au ingia katika tovuti ya Baraza la Mitihani ili utengeneze 'Control number' ya kufanyia malipo kwa utaratibu ulioelekezwa.
 - (c) Fanya malipo ya ada ya Mtihani kupitia Posta au Benki kwa kutumia 'Control Number'.
 - (d) Fika Posta kufanya usajili au jisajili mwenyewe kupitia tovuti ya Baraza la Mitihani kwa kufuata hatua zilizooneshwa kwenye tovuti.

- (e) Baada ya usajili kukamilika chapa na wasilisha nakala **moja** ya fomu Ofisi ya Posta, wasilisha nakala ya **pili** kwenye Kituo utakachofanyia Mtihani na nakala ya **tatu** ya fomu itunzwe na wewe (mtahiniwa) mwenyewe kwa ajili ya kumbukumbu.
5. Ufafanuzi kuhusu utaratibu wa hatua za kufuata katika usajili, umetolewa katika tovuti ya Baraza la Mitihani www.necta.go.tz. Waombaji wote **wanasisitizwa** kuhakikisha wanajisajili mapema kwani mfumo wa usajili utafungwa baada ya kipindi cha usajili kumalizika.

Imetolewa na;

KATIBU MTENDAJI